

BUNGE LA TANZANIA

---

MAJAADILIANO YA BUNGE

---

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 19 Julai, 2012

(Mkutano Ulianza Saa Tatoo Asubuhi)

D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**Kusimamishwa Shghuli za Bunge Kutokana na Kuzama  
Meli**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutumie dakika chache tusimame tuweze kuwakumbuka wenzetu waliopoteza maisha kutokana na ajali iliyotokea jana. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za Marehemu mahali pema Peponi. Amen.

*(Hapa Wabunge Walisimama dakika chache  
kuwakumbuka waliopoteza maisha kutokana na ajali  
ya  
Meli ya MV. Skagit)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, napenda nitoe taarifa fupi ya majonzi na masikitiko kufuatia ajali ya meli iliyotokea jana Zanzibar. Kama tulivyoosikia wote, jana meli ya M.V. *Skagit* yenyeye usajili wa Zanzibar ilipinduka na kuzama katika Kisiwa kidogo cha Chumbe karibu na Bandari ya Zanzibar.

Kwa taarifa zilizopo, meli hiyo ilikuwa na abiria 290 wakiwemo watu wazima 250, watoto 31 na crew tisa. Baada ya ajali hiyo, shughuli za uokoaji zilianza mara moja na hadi leo asubuhi watu waliookolewa waliokuwa hai ni 146 na waliookolewa wamekufa, yaani maiti ni 31 na wote maiti 31 wametambuliwa na ndugu zao. Kati ya hao waliookolewa wakiwa hai 146 ndani yake, ndani ya meli kulikuwa na watalii 16. Kwa hiyo, watalii 14 kati ya hao 16 wameokolewa wakiwa hai na katika wale maiti 31, mmoja ni mtalii na mwingine anatafutwa. Idadi ya wale wanaoendelea kutafutwa ni 113 ambapo shughuli jana zilisimamishwa kidogo kutokana na machafuko ya hali ya hewa, lakini leo shughuli za kuwatafuta wengine katika ile meli zinaendelea.

Kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara na Serikali ya Jamhuri ya Muungano imetangaza siku tatu za maombolezo na Serikali ya Mapinduzi vilevile yenye we imetangaza siku tatu za maombolezo. Lakini kwa sababu hii meli pia inawezekana ikawa na abiria kutoka Bara, kwa ndugu wote ambao wanataka kujua habari za ndugu zao waliopata ajali katika meli hii kwa upande wa Tanzania Bara, kituo cha mawasiliano na maelezo itakuwa ni Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba niseme hii ndiyo taarifa ya awali na utaratibu wa mazishi umeshapangwa kule Zanzibar, ndugu wanaendelea na mazishi yanayofanyika leo kwa wale watu waliofariki. Kama nilivyosema, vikosi vyetu na jitihada mbalimbali zikisimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano inaendeleza jitihada za kutafuta wale waliobaki katika ile meli ambayo idadi yao mpaka leo ni 113.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa ya awali.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu, tunaomba tuwape pole sana ndugu zetu waliopotelewa na ndugu zao kutokana na ajali hii. Lakini jana tuliweza kuwapeleka wenzetu 18, wako Zanzibar saa hizi na Maafisa wetu wengine wanakwenda kusimamia kule. Lakini kwa sababu bado tunaendelea kufuatilia hili suala, tumekubaliana kwa vyovyote vile Waheshimiwa Wabunge wote posho ya siku moja tutaichukua kusudi tuweze kusaidia matatizo yaliyoko kule Zanzibar.

Pia tumekubaliana katika Kamati ya Uongozi kwamba hatuna budi, hali iko tete kila mahali na watu wanajaribu kufuatilia ndugu zao wako wapi, kwa hiyo tutaahirisha kikao cha leo, hatutafanya Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi, tukiendelea kupata habari nyingine zozote.

Tulikuwa tunaamini kwamba pengine kutakuwa na mazishi ya halaiki, lakini kufuatana na Serikali ya Mapinduzi, wamesema hapana mpaka sasa, kwamba wale walioweza kupatikana, maiti wametambuliwa na ndugu zao na meli imechukuliwa na ndugu zao. Lakini ukiangalia ile idadi ya wale ambao hawajapatikana ni kubwa.

Kwa hiyo, hatuwezi kukwepa kabisa kwamba pengine inaweza ikatokea pawepo na mazishi ya halaiki. Kwa hiyo, kwa leo naomba niahirishe kikao cha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 3.08 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 20 Julai, 2012, Saa Tatu Asubuhi)*